
# Maswali Yetu Muhimu kwa Serikali ya Tanzania



# MASWALI YETU MUHIMU KWA SERIKALI YA TANZANIA

MASWALI YETU MUHIMU KWA SERIKALI YA TANZANIA

Kimetayarishwa na Kikundi Kazi cha Bajeti cha Policy Forum

Mchora Katuni: Regis Maro

Kimechapishwa na Policy Forum

Toleo la Kwanza: Oktoba, 2015

ISBN: 978-9987-708-19-2

Kimesanifiwa na kupigwa chapa na;

JAMANA PRINTERS

# Yaliyomo


1. Utangulizi .......................................................ii
2. Muhtasari .......................................................iii
3. Ukusanyaji wa rasilimali za ndani ............................. 1
4. Maji ............................................................... 3
5. Elimu ............................................................. 6
6. Afya ............................................................... 7
7. Haki ya Ardhi ..................................................10
8. Kilimo ...........................................................12
9. Hitimisho .......................................................14

# Utangulizi

*Mfumo wa Uongozi / utawala wa sasa wa Tanzania utafikia mwisho wake katika siku chache zijazo. Hii inatoa njia kwa mfumo mpya utakaochukua hatamu inategemewa kuwa na mikakati mipya au iliyoboreshwa kusukuma maendeleo ya kiuchumi. Kwa uelewa kwamba chama chochote kitakachofanikiwa kushika uongozi (baada ya uliopo sasa) kitakuwa tayari na ilani yake sisi Kikundi Kazi cha Bajeti chini ya Policy Forum, tunapenda kutoa wito kwa serikali ijayo kujitoa kwa masuala muhimu yaliyowasilishwa ambayo tunafikiria, kama yakizingatiwa katika utekelezaji kuna uwezekano wa kuona maendeleo dhahiri katika maisha ya watu wa Tanzania.*

***Semkae Kilonzo***

*Mratibu, Policy Forum*

## Muhtasari

Ufuatao ni muhtasari wa vipaumbele muhimu ambavyo serikali inatakiwa kuzingatia.

### 1. Ukusanyaji wa rasilimali za ndani

i. Kuandaa mpango wa utekelezaji wa kuleta mabadiliko katika sera ya fedha kupambana na upotevu wa kodi unaotokana na ukwepaji wa kimfumo wa kodi, ulipaji wa kodi ndogo kuliko inavyopasa na utoroshaji nje ulio haramu unaokausha rasilimali za ndani.

ii. Kutengeneza pendekezo thabiti kuhusu upitiaji na upigaji chapa mikataba yote katika sekta ya uziduaji ili kuachia njia kwa ulipaji stahiki wa kodi na unufaikaji kutokana na sekta ya uziduaji.

iii. Kusaidia uanzishwaji wa chombo cha uratibu wa kodi baina ya vitengo mbalimbali ndani ya serikali.

iv. Kupanga upya muundo wa Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA) ili kuboresha ufanisi, uwazi, na uwajibikaji katika ukusanyaji wa kodi.

v. Kutengeneza mwongozo wa kisera wa uanzishwaji wa regista (uandikishaji) ya makampuni wenye tija na unaomilikiwa na umma.

### 2. Maji

i. Kuendeleza kasi nzuri ya utoaji wa fedha za ndani kwa ajili ya maji na usafi wa mazingira.

ii. Kuhimiza utawala bora na uwajibikaji kwa ajili ya maji na usafi wa mazingira.

iii. Kuunganisha maji na usafi wa mazingira katika sera za afya, mikakati na mipango.

### 3. Elimu

i. Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

ii. kurejesha hadhi ya Mwalimu.

iii. kuwekeza zaidi kwenye miradi ya maendeleo

## 4. *Afya*

i. Kuboresha utoaji wa fedha za huduma ya ya afya kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii. (CHF/TIKA.)

ii. Kuongeza utoaji wa fedha kwa ajili ya rasilimali watu wa huduma za afya

iii. Kuongeza utoaji fedha kwa ajili ya vifaa vya afya

iv. Kuimarisha Mfuko wa UKIMWI (AIDS Trust Fund) kuhakikisha huduma bora dhidi ya UKIMWI.

v. Kuboresha miundombinu ya afya.

## 5. *Haki ya ardhi na utunzaji misitu*

i. Kuweka na kutimiza haki ya wanawake juu ya ardhi.

ii. Kuboresha maisha vijijini kupitia kilimo.

iii. Kuhakikisha sera na sheria ya misitu inatekelezwa kwa vitendo.

iv. Kuanzisha na kusimamia utekelezaji wa mipango wa matumizi bora ya ardhi za vijiji.

v. Kusisitiza uboreshwaji wa utawala na uwajibikaji katika sekta ya misitu kwenye ngazi zote.

## 6. *Kilimo*

i. Kuhimiza ukuaji uchumi wenye ufanisi unaoongozwa na kilimo.

ii. Kuhakikisha wakulima wadogo wanafikia mikopo kwa urahisi.


iii. Juhudi za kimkakati kuwezesha wanawake na jamii vijijini kulima kwa ufanisi.

iv. Kuingiza mikakati ya kukabiliana na changamoto za kilimo katika mipango ya Wilaya na kutenga rasilimali kwa utekelezaji.

v. Kubuni na kutekeleza mipango kwa ajili ya wanawake kujiongezea uwezo wa kunyumbulika pia kushiriki katika majadiliano na mipango ya mabadiliko ya tabianchi.

# 1. UKUSANYAJI WA RASILIMALI ZA NDANI

Kwa kufuatana na Mwalimu Nyerere “uhuru ni kuhusu kujitegemea”. Tanzania kama taifa linahitaji kutumia rasilimali zake zenyewe zilizopo kwa ajili ya maendeleo yake binafsi. Hivi sasa, karibu asilimia 15 ya bajeti ya taifa hutegemea wahisani. Wahisani wanapozuia misaada yao, shughuli za maendeleo hukwama, hivyo juhudi zinahitajika kuongeza kwa dhahiri ukusanyaji wa rasilimali za ndani. Inaonekana, Tanzania inahitaji uwekezaji zaidi katika kuendeleza miundo mbinu, lakini nchi tayari ina deni kubwa. Tanzania ni tegemezi sana kwa kodi - kodi ya ongezeko la thamani ambayo ni asilimia 24 ya mapato yanayotokana na kodi katika bajeti ya serikali. Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) hulipwa zaidi na Watanzania walio maskini kutokana na matumizi ya bidhaa na huduma. Makampuni ya kimataifa yanafurahia misamaha ya kodi ya VAT kupitia mikataba ya kutatanisha, serikali iliyowekeana saini nao. Ukwepaji kodi na ulipaji kodi kidogo kuliko inavyopaswa ni mkubwa sana, utoroshaji haramu wa fedha hunyima nchi rasilimali fedha inayohitajika sana kwa maendeleo. Kwa mfano, shirika la “Global Financial Integrity” limekadiria kuwa Tanzania ilipoteza euro bilioni 2.5 kwa mwaka 2002-2011 peke yake kwa ajili ya bei zisizo halali kibiashara na katika uhawilishaji fedha unaofanywa na makampuni ya kimataifa.



## Fursa Zilizopo

Mwezi Februari 2015, Rais Kikwete aliamua kuifanyia kazi taarifa ya jopo la Maofisa wa Ngazi ya Juu wa Umoja wa Afrika kuhusu utoroshwaji haramu wa fedha kutoka bara la Afrika. Miongoni mwa makubaliano hayo ni pamoja na taratibu / kanuni imara, rasilimali zaidi, uwezo na uwazi, Ilikuwepo na kuzitaka nchi za Afrika kudhibiti motisha za kodi zenye madhara wanazopewa wawekezaji wa nje.

Taarifa hiyo hiyo inapendekeza Tanzania idhibiti mtiririko haramu wa fedha unaotokana na rushwa na miundo ya umiliki iliyofichika. Taarifa kama zile zilizovuja Februari 2015 kutoka benki ya Kiswizi ya HSBC (Swiss HSBC-bank) zinaonyesha kwamba hata Watanzania matajiri huficha mali zao ili kukwepa kodi. Taarifa zilionyesha Watanzania 99 walikuwa na dola milioni 114 katika benki ya Uswizi wakati habari hizi zilipovuja. Pia ni ukweli kwamba Ajenda ya Utekelezaji ya Addis inaweka umuhimu mkubwa zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kugharamia malengo ya maendeleo endelevu (SDGs).

**Kwa maelewano haya tunaisihi Serikali ije na:**

1) *Mpango wa utekelezaji wa kuleta mabadiliko ya kimfumo katika sera ya fedha ili kupambana na upotevu wa kodi unaotokana na mfumo wa ukwepaji kodi, ulipaji kodi mdogo kuliko inavyopasa na njia zingine haramu za utoroshwaji zinazokausha rasilimali za ndani. Hili lijumuishe mikataba ya utozwaji kodi maradufu na mikataba ya kibiashara yenye vifungu vya kodi.*

2) *Pendekezo madhubuti katika upitiaji na uchapishaji wa mikataba yote katika sekta ya uziduaji ili kutoa njia kwa kodi stahiki na yenye tija kutokana na sekta ya uziduaji.*


3) *Kuwezesha uanzishwaji wa chombo cha kodi baina ya vitengo mbalimbali ndani ya serikali kitakachokuwa na jukumu la kufanyia kazi sera za kimataifa badala ya Chombo cha sasa cha Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD) ambacho hakijumuishi kwa usawa nchi zote, ikiwemo Tanzania.*

4) *Kupanga upya muundo wa TRA ili kuboresha ufanisi, uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa kodi*

5) *Kuhakikisha kuwa serikali inatumia mapato ya kodi kwa lengo la kuliletea Taifa mendeleo.*

## 2. MAJI

Watanzania bado wanaweka maji na usafi wa mazingira kama kipaumbele cha juu katika mahitaji yao ya kimaendeleo.Lakini mahitaji hayo hayajaweza kufikiwa mwaka hadi mwaka. Kwa ulinganisho Tanzania haipo katika mkondo wa kufikia malengo ya maendeleo ya millennia (MDGs) ya maji na usafi wa mazingira, licha ya maendeleo yaliyopatikana chini ya Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji (WSDP1). Mchanganuo wa mahitaji ya fedha na utengaji wa bajeti zinaonyesha kuwa hata ongezeko la hivi karibuni katika utolewaji wa fedha kwenye sekta hiyo bado ni nusu ya mahitaji halisi kufikia malengo hayo.  Pamoja na maendeleo mazuri yaliyopatikana katika awamu ya kwanza ya Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji, bado kuna vizingiti muhimu vya kufanyia kazi kwa mabadiliko endelevu. Tumebainisha vizingiti muhimu kama vitano katika sekta ya Maji na Mazingira Tanzania, na tunaisihi Serikali ifanyie kazi;



a) **Kuendeleza kasi nzuri katika utoaji wa fedha za ndani kwa ajili ya Maji na Usafi wa Mazingira (WASH)**

Utoaji wa fedha za ndani kwenye bajeti ya sekta ya maji uliendelea kuongezeka katika mwaka wa fedha 2014/15 kitarakimu na kama sehemu ya jumla ya bajeti ya sekta. Hivyo ni kiashiria kizuri kuonyesha dhamira ya Serikali kuboresha ufikiaji wa huduma ya maji. Mgawo wa bajeti ya kisekta inayotoka ndani ya nchi kwa mwaka wa fedha 2014/15 ni asilimia 66 ikilinganishwa na asilimia 51 ya bajeti iliyoidhinishwa ya mwaka wa fedha uliopita.[1] Japo hii ni hatua nzuri ya kupongezwa kwa sekta ya maji, lakini sekta ndogo ya usafi wa mazingira hupata fedha kidogo sana toka serikalini. Hivyo, tunatoa wito kwa Serikali kuendeleza kasi hii ya kuongeza utoaji fedha kwa ajili ya maji na usafi wa mazingira (WASH) na kupunguza utegemezi kwa nchi za nje.

b) **Kukuza Utawala Bora na Uwajibikaji kwa ajili ya Maji na Usafi wa Mazingira (WASH)**

Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji (WSDP) umeonyesha matokeo yaliyokuwa chini ya matarajio na manufaa madhubuti machache kwa Watanzania walio masikini. Ufuatiliaji wa utendaji na uwajibikaji kifedha umeonekana kuwa dhaifu, na ubora wa majadiliano ya kisekta yamedhoofu. Ufikiaji wa malengo ya utawala bora na uwajibikaji umekuwa wa taratibu. Kukuza na kuwezesha uendelevu kimaendeleo umekuwa ni suala nyeti katika utoaji wa huduma ya maji, na usafi wa mazingira. Serikali na wadau wengine, pamoja na wahisani wanatoa umuhimu mdogo katika kulifanyia kazi. Kwa kuelewa kuwa uwajibikaji kisekta ni kipengele muhimu katika ufanisi wa utoaji huduma. Tunatoa wito kwa Serikali kuhakikisha kuwa maamuzi yanafanywa kuitikia wito wa mahitaji ya maji na usafi wa mazingira (WASH) kwa wanajamii masikini.

---

1 Rapid Budget Analysis for the Water Sector

### c) Kuingiza WASH katika sera ya afya, mikakati na mipango

Upunguzaji wa vifo vya akina mama wajawazito na wanaonyonyesha, watoto wanaozaliwa, na watoto wadogo ni kipaumbele kwa wote, kwa kuzingatia kiwango cha juu cha magonjwa na vifo vya akina mama, watoto wanaozaliwa na watoto wadogo katika miongo miwili iliyopita katika nchi za kiafrika, Tanzania ikiwemo. Hii ni mojawapo ya masuala muhimu yanayofanyiwa kazi ulimwenguni na kitaifa kama inavyoonyeshwa katika Malengo ya Maendeleo ya Milennia, Maono ya Tanzania (Tanzania Vision) 2025, na Mpango Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania -MKUKUTA), na Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi -MMAM), kati ya mingine. Maji, Usafi wa mazingira (WASH) na afya hivyo zitakuwa zinachangia katika mpango huu wa serikali, zikisisitiza umuhimu wa kuhakikisha WASH inajumuishwa katika mipango /miradi inayobuniwa kupunguza vifo vya akina mama na watoto wanaozaliwa.

Tafiti zimeonyesha kuwa, upatikanaji wa miundombinu ya kusafisha mikono Tanzania ni duni, hususan katika vituo vya afya. Hospitali/ vituo vya afya/zahanati nyingi hazina sehemu za kusafishia mikono na upatikanaji wa maji safi na salama ni suala nyeti hasa katika wodi za akina mama zisizo na kitengo cha upasuaji. Kuhusu usafi wa mazingira, kuna kiwango kidogo cha usafi wa vitanda vya kuzalia, vyoo vya wagonjwa, na vifaa vya kusafishia. Hali hii inaelekea kuhusiana na uhaba wa watumishi na kutokuwepo mafunzo kwa wahudumu wa afya. Bado kuna changamoto katika masuala ya utunzaji vyoo, maji na uondoaji wa taka ngumu[2]. “Serikali inapaswa iimarishe haki za wanawake na kuboresha afya za wanawake, wasichana, na watoto wa Tanzania” hasa kwa kuimarisha kiwango cha ubora wa huduma za akina mama kwa kutoa huduma toshelevu za WASH katika hospitali/vituo vya afya/zahanati hususan katika wodi za akina mama.


2 WaterAid (2014) Improving Maternal and Newborn Health in Zanzibar; *A need assessment of IPC and WASH across maternity units*

# 3. ELIMU

## Nini kifanyike kuboresha maendeleo katika sekta ya Elimu?

### a) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia

Hali ya shule za msingi na sekondari si ya kuridhisha kwa wanafunzi. Takribani asilimia 35 wanakaa chini, madarasani bado wamerundikana ambapo uwiano wa darasa kwa wanafunzi ni 72 badala ya 40, bado kuna uhaba mkubwa wa vyoo ambapo uwiano hivi sasa ni wanafunzi 52 kwa tundu moja badala ya wanafunzi 25 kwa tundu la choo. Elimu bora italetwa na mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia hivyo tunahitaji Serikali iboreshe mazingira ya kufundishia na kujifunzia ya shule za msingi na sekondari.




### b) Kurejesha hadhi ya Mwalimu

Walimu wamekuwa na migogoro na serikali kwa muda mrefu kutokana na madai yao, mishahara midogo, ukosefu wa motisha na mazingira duni ya makazi na kufanyia kazi. Kutokana na hali hii asilimia 66 ya walimu hawafundishi ipasavyo kwa ama kutoingia kwenye kipindi au kuingia na kufundisha kwa nusu ya muda uliopoangwa (Twaweza,

2014) na pia walimu hawajiandai ipasavyo kufundisha kwa mujibu wa mihutasari ya masomo (HakiElimu 2015). Hivyo tunahitaji kiongozi ajaye abainishe azma ya kurejesha hadhi ya walimu na mkakati wake ili kada ya walimu iweze kuwa na walimu mahiri na wanaofundisha ipasavyo.

### c) Uwekezaji kwenye miradi ya maendeleo

Changamoto nyingi za sekta ya elimu zinatokana na uwekezaji mdogo wa miradi ya maendeleo ya sekta ya elimu. Kwa kipindi cha miaka kumi bajeti ya maendeleo ya sekta ya elimu imekuwa ni asilimia kati ya 12-16 tu ya bajeti nzima ya sekta ya Elimu. Fedha nyingi zinatumika kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo na mikopo ya elimu ya juu. Hivyo ili kutatua changamoto za mazingira ya kufundishia na kujifunzia tunahitaji kiongozi ajaye aweke dhamira ya kuongeza bajeti ya maendeleo ya sekta ya elimu kufikikia asilimia 30 ya bajeti ya sekta ya elimu. Lazima kuwe na azimio la kutenga asilimia 20 ya bajeti ya taifa kwenye sekta ya elimu tofauti na ilivyo sasa ambapo bajeti ya sekta ya elimu ni asilimia 17 ya bajeti ya taifa.

## 4. AFYA

### a) Utoaji wa Fedha za Afya

Hivi sasa , Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imetayarisha Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya (MMSA IV) wenye gharama za mwaka zinazokisiwa kuwa kati ya Tsh. Bilioni 4 kwa mwaka 2015/16 hadi Tsh. Bilioni 4.9 kwa mwaka 2019/20. Kwa kuzingatia vyanzo vyote vya fedha (ndani na nje ya bajeti, na ndani na nje ya nchi), kuna pengo la asilimia 41 linalobakia. Hili pengo litahitaji ama kulipiwa kwa fedha za mfukoni zinazotoka (kwa walio masikini na waishio katika mazingira magumu) au ubora na idadi ya huduma zitakuwa pungufu ya zilivyopangwa.

Tunatoa wito kwa uboreshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF/TIKA) na utengaji wa bajeti kwa ajili ya misamaha kama hatua za muda mfupi wakati bima ya afya ya kisheria ikitayarishwa. Pia tunatoa wito wa ongezeko la utoaji

wa fedha toka mfuko wa jumla ili kupunguza pengo la utoaji wa fedha ambalo linaathiri zaidi wale walio fukara. Tunapendekeza kuwa Serikali itenge kiwango cha fedha kilicho na uhalisia kwa sekta ya Afya.




## b) Vifaa Tiba

Kwa miaka minne iliyopita utengaji wa fedha kwa ajili ya madawa muhimu na vifaa vya afya umekuwa mdogo sana. Ingawaje utengaji fedha kwa mwaka wa fedha 2011/12 ulikuwa Tsh. Bilioni 123.4, upungufu wa vifaa kwa mwaka 2012 ulibainishwa kuwa kiasi cha asilimia 60. Lakini hali haielekei kuboreka kwa siku za usoni. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, Wizara yaAfya na Ustawi wa Jamii (MoHSW) ilitenga kiasi cha Tsh. bilioni 36.2 peke yake kwa ajili ya madawa muhimu na vifaa tiba wakati makisio ya mahitaji ni Tsh. bilioni 577. Makisio haya hayaendani na malengo ya Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ya kufikia asilimia 80 uwepo wa bidhaa ifikapo 2016. Kadhalika bajeti pia ilishindwa kuzingatia ukuaji wa idadi ya watu, idadi ya vituo vipya vya afya, mzigo wa maradhi na mahitaji halisi. Bajeti itakuwa na matokeo hasi katika utoaji wa huduma za afya na itaongeza mzigo wa upungufu wa fedha kwa wananchi. Kwa hiyo tunatoa

wito wa ongezeko la fedha kutoka serikali kuu na serikali za mitaa (CHF/TIKA) ili kuondoa pengo kubwa lililopo sasa.

### c) Rasilimali Watu Kwa Afya

Watumishi wa Afya waliopo ni kama nusu ya idadi ya wanaohitajika. Wakati huu wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inakisia uwepo wao kuwa watumishi 15 kwa watu 10,000, wakati Shirika la Afya Duniani (WHO) inapendekeza uwiano wa watumishi 23 kwa idadi ya watu 10,000 kwa nchi zinazoendelea.

Tunatoa wito kwa ongezeko la fedha za mafunzo kwa kada zote, maandalizi ya ajira na udumifu wa uwepo wao. Pia uboreshaji wa mazingira ya kazi ni muhimu; kwa mfano upatikanaji wa madawa na vifaa tiba, nyumba, malipo kwa wakati, usimamizi (utawala bora) na menejimenti ya utendaji ni mambo ya muhimu kuhakikisha udumifu wa watumishi wa afya, hususan vijijini na katika maeneo yenye watumishi wachache.

### d) UKIMWI

Hivi sasa utoaji fedha kwa shughuli za UKIMWI hufanyika zaidi kwa kupitia misaada ya wafadhili wa nchi za nje, lakini wahisani wameanza kujitoa taratibu au kupunguza kiasi cha ufadhili. Hali hii inaelekeza katika wito wa upatikanaji wa vyanzo mbadala vya fedha. Mfuko mpya wa UKIMWI ulioanzishwa hivi karibuni unahitaji kuimarishwa ili kuweza kupata fedha za kutosha na kuzisimamia ipasavyo. Tunatoa wito kwa ongezeko la utoaji wa fedha za ndani ya nchi.


### e) Miundombinu ya Afya

Ufikiaji wa huduma bora za afya vijijini siyo kamilifu kutokana na uhaba wa vituo vya afya na hospitali. Kiasi cha asilimia 60 ya vituo vya afya vyote na asilimia 47 ya hospitali zipo vijijini, ambapo asilimia 70 ya Watanzania wanaishi. Hivyo basi, ni vizuri upatikanaji wa bidhaa, vifaa na watumishi wa afya uende sambamba na uboreshwaji wa ufikiaji wa huduma za afya ya msingi, pamoja na ujenzi na ukarabati wa hospitali na vituo vya afya.

# 5. HAKI YA ARDHI

Misitu ni rasilimali muhimu sana ambayo nchi yetu imejaliwa. Inakadiriwa Tanzania ina misitu yenye ukubwa wa hekta millioni 48.1 ambayo ni sawa na asilimia 38 ya eneo lote la ardhi ya nchi yetu. Asilimia 31 ya misitu yote ipo chini ya uhifadhi, katika ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na ngazi ya Serikali Kuu, Serikali za Wilaya na Serikali za Vijiji. Asilimia 69 ya misitu iliyobaki ipo katika ardhi za Vijiji na kwenye maeneo ya wazi.

Pamoja na juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali na wadau wengine ikiwa ni pamoja na wanavijiji na mashirika yasiyo ya kiserikali, bado hali ya misitu yetu ni mbaya. Inakadiriwa Tanzania hupoteza wastani wa hekta 400,000 za misitu kila mwaka (Ripoti ya Naforma 2013).




## a) Kilimo cha Biashara na Haki za Wakulima Wadogo wadogo

Katika nchi nyingi pamoja na Tanzania, ardhi imekuwa ya kibiashara kutokana na mashinikizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ongezeko la idadi ya watu na ongezeko la mahitaji ya chakula na bidhaa nyinginezo ulimwenguni.

Nchini Tanzania, matumizi mapya ya ardhi kwa uzalishaji wa nishati ya mimea, chakula kwa ajili ya mauzo nje ya nchi, uziduaji wa madini, mafuta na gesi na upanuzi wa kilimo cha biashara; vimeongeza ushindani juu ya ardhi na rasilimali zinazotokana na ardhi. Kuna matokeo yenye athari kubwa kwa wanajamii walio wengi vijijini wanaopoteza rasilimali pamoja na uwezo wa kufanya maamuzi. Hili pia limechangia kwenye uhaba wa chakula kwani kilimo kwa wazalishaji wadogo ni muhimu na ni msingi wa kupata chakula na fedha kwa matumizi mengine ya msingi kama huduma za afya na elimu. Tunapenda Serikali kuhakikisha kuwa Wakulima wadogo wananufaika kutokana na uwekezaji katika ardhi kwa kuzingatia usawa na haki zao za kupata chakula zinalindwa. Mapatano ya kibiashara kuhusu ardhi yawe wazi na taratibu husika zifuatwe.

## b) Haki za Wanawake Kuhusu Ardhi

Hivi sasa wanawake nchini Tanzania wanakumbana na changamoto nyingi katika kupata haki zao zihusianazo na ardhi. Hii inatokana na:

i. Uwili katika mfumo wa umiliki wa ardhi: Kwamba mfumo wa umiliki wa ardhi wa kiasili unaendeshwa sambamba na mfumo wa kisheria ambapo ule wa kwanza unatawaliwa zaidi na wanaume.

ii. Ukosefu wa elimu kuhusu haki za wanawake miongoni mwa wanawake na umma kwa ujumla.

iii. Ubaguzi na fikra hasi kuhusu uwezo wa wanawake, umahiri, cheo n.k.

iv. Mila za kizamani, desturi na imani za kidini zinazobagua wanawake katika kupata usawa katika umiliki wa rasilimali za uzalishaji mali.

Tunapenda Serikali ihakikishe haki za wanawake Tanzania katika umiliki kwa njia ya:

i. Utengaji wa rasilimali za kutosha kwa ajili ya mwamko mpana kwa umma kuwezesha wanawake kuimarisha elimu juu ya haki yao ya kumiliki mali.

ii. Toa madaraka ya utawala wa ardhi mikoani /wilayani ili kuruhusu jamii zilizoko kwenye ngazi za msingi vijijijni (ambapo wanawake wengi wako) kushiriki katika maamuzi.

iii. Kujenga uwezo wa kiuchumi wa wanawake kuwawezesha kushiriki katika ushindani wa kibiashara kuhusu ardhi.

iv. Utaalamu wa kijinsia katika Ushiriki wa Matumizi ya Ardhi na Menejimenti (PLUM) katika ngazi ya wilaya na wanawake wawe ni sehemu ya kamati mbali mbali za hukumu za kesi za ardhi.

**c) Boresha maisha vijijini kwa njia ya kilimo**


Hivi sasa, matumizi ya pembejeo za kilimo ni ndogo sana. Tanzania inatumia kilo 9 kwa hekta ya mbolea na kiasi cha asilimia 10 ya wakulima wanatumia mbegu bora. Kiwango kidogo cha teknolojia, utegemezi mkubwa kwa kilimo cha mvua, upungufu wa huduma za ugani za kilimo, uzalishaji mdogo wa nguvu kazi, miundo mbinu zisizotosheleza za usafirishaji na masoko, ni vikwazo muhimu vinavyozuia ukuaji wa haraka wa sekta. Tunapenda Serikali kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani na mikopo.

## 6. KILIMO

Tanzania ina uwezo mkubwa ambao haujadhihirika wa ukuaji wa uchumi uongozwao na kilimo. Nchi ina ardhi kubwa na rasilimali maji, wajasiria mali wa kilimo wenye motisha na bandari kubwa ya kuwezesha kufikia masoko ya nje. Wanawake wanashiriki kikamilifu katika mnyororo wote wa thamani na wamejengewa uwezo kama wanufaika.

Hali ya hewa ni nzuri kwa mazao ya aina mbali mbali na kwa kuongeza kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya mbegu bora, kiwango cha uzalishaji kinaweza kuongezeka kwa haraka.

Leo, karibu asilimia 80 ya watanzania wameajiriwa kwenye sekta ya kilimo, ambacho kinatoa nusu ya mapato ya taifa na robo tatu ya bidhaa zinazouzwa nchi za nje.




Kwa kuzingatia mchango mkubwa ambao sekta ya kilimo inatoa kwa uchumi wa Tanzania, kuna hisia kwamba sekta hii haijapewa kipaumbele kinachostahili. Kwa hiyo tunatoa wito kwa Serikali:

i. Kukuza ukuaji uchumi unaoongozwa na sekta ya uchumi.

ii. Kuhakikisha kuwa wakulima wadogo wanafikia mikopo.

iii. Fanya juhudi za kimkakati kuwezesha wanawake na wanajamii vijijini kulima kwa ufanisi.

iv. Ingiza mipango ya kukabiliana na hali katika mipango ya wilaya na tenga rasilimali za utekelezaji.

v. Kubuni na kutekeleza mbinu za kukabiliana na hali na kwa wanawake kuongeza uwezo wao wa kunyumbulika, pia kushiriki katika majadiliano na mipango kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

## Hitimisho

Inawezekana Serikali kuboresha mfumo wa kodi na kuweza kukusanya mapato ya kutosha kugharamia kwa kiwango kikubwa miradi yake ya maendeleo. Ukusanyaji wa mapato ya kutosha sharti uende sambamba na uhalisia pamoja na uwajibikaji katika matumizi ya hizo rasilimali.

Masuala tuliyowasilisha hapa yanahitaji dhamira ya hali ya juu katika kuyafanyia kazi. Kwa bahati nzuri, maeneo yaliyoainishwa kama yakifanyiwa kazi vizuri yana matokeo ya moja kwa moja katika maisha ya watu wetu wengi. Wanaweza kufaulu haraka pale wanapokidhi matakwa ya watu walio wengi. Tunategemea Serikali itachukulia mapendekezo haya kwa umakini na kuyaingiza katika mipango yake mbali mbali ya kimaendeleo.

policy forum

Plot 14, Sembeti Road
Mwai Kibaki Road
P.O. Box 38486, Dar es Salaam
Tel: +255 22 2780200
Website: www.policyforum.or.tz
Email: info@policyforum.or.tz